MWITO PROG 1074 KISWAHILI SCRIPT

SCRIPTURE: ROMANS 4:10

TRANSWORLD RADIO

INTRO:

Nakukaribisha tena mpendwa msikilizaji wangu kwa kipindi cha MWITO nambari 1074 kutoka studio zetu za Nairobi. Sina shaka kuwa Mungu amewalinda n ahata kuwafikisha siku ya leo tangu tulipokutana mara ya mwisho kwenye kipindi kilichopita.

Nakukumbusha kuwa kipindi hiki kinakujia kwa hisani ya huduma ya kimataifa ya Macedonia Call yake mchungaji Harold Williams. Kwa dakika 15 zijazo utafaidika kutokana na neno kutoka kwa huduma yake mchungaji Harold Williams. Hii ni sehemu muhimu ya mtumishi huyu wa Mungu ambaye amekuwa akishiriki nanyi kwa miaka kadhaa iliopita neno la Mungu. Ikiwa ungependa kupokea maelezo Zaidi kuhusu huduma hii, naomba uwasiliane nami kwa anwani nitakayokupatia mwishoni mwa kipindi hiki. Ninaamini kwamba baada ya kusikiliza hiki tutazidi kuwasiliana. Jinsi ilivyo kawaida yangu msikilizaji singependa kukuwacha kwenye giza kuhusu tunakotoka na tunakoelekea. Nakupa tu muhtasari maandiko tuliosoma kwenye kipindi kilichopita, kisha tuendelee. Tulisoma aya za 8-9 za kitabu cha Warumi ifwatayo: **Je? Uheri huo ni kwa hao waliothiriwa, au kwa hao pia wasiotahiriwa? Kwa kuwa twanena ya kwamba kwake Ibrahimu Imani yake ilihesabiwa kuwa ni haki. Alihesabiwaje basi? Alipokwisha kutahiriwa au kabla ya hajatahiriwa? Si baada ya kutahiriwa bali kabla ya kutahiriwa.**

Kwa wale ambao hamukuwa nasi kwenye somo lililopita angalau mmepata picha kuhusu tulichokuwa tukizungumzia. Maandiko yanasema kwenye aya ya 10 kwamba: **Alihesabiwaje basi? Alipokwisha kutahiriwa au kabla ya hajatahiriwa? Si baada ya kutahiriwa bali kabla ya kutahiriwa. Naye aliipokea dalili hii ya kutahiriwa, muhuri ya ile haki ya amani aliyokuwa nayo kabla hawakutahiriwa, ili na wao pia wahesabiwe haki; tena awe baba ya kutahiriwa kwa wale ambao si waliotahiriwa, kwa wale ambao si waliotahiriwa tu, bali pia wanazifwata nyayo za Imani baba yetu Ibrahimu aliyokuwa nayo kabla ya kutahiriwa.**

Naam msikilizaji wangu kwa ufupi ni kwamba hapa mtume Paulo anajaribu kutueleza msingi wa ukweli kwamba Mungu si wa kuheshimu watu, vitu au hali.

Kwamba Mungu alimhesabia Ibrahimu haki kitambo sana na Ninaamini ukichunguza historia ya Bibilia ni baada ya 14 baada ya maandiko kusema kuwa Ibrahimu alimwamini Mungu na alihesabiwa haki baada ya miaka 14. Kwamba Ibrahimu alitahiriwa kama muhuri na ishara ya Imani ambayo aliitisha miaka kadhaa ya nyuma. Paulo analeta hali hiyo ili tuweze kuona kanuni muhimu kwenye aya ya 10, kwamba ili Ibrahimu awe Baba wa wale watakaoamini, hata hawatakuwa wametahiriwa, watahesabiwa haki na wao. Ikiwa maandiko yangehusisha kutahiriwa na kuhesabiwa haki, jambo hilo lingezua utata mwingi, huku watu wakitafuta kufwata mkondo. Kwa sasa kwa kuwa maandiko yanasema ili Ibrahimu ahesabiwe baba wa kila mtu aaminiye kwenye Wagalatia sura ya 3: tunaambiwa kuwa sisi tu watu wa Baba yetu Ibrahimu, Wa mbegu ya kiroho ya Ibrahimu, Kwamba Ibrahimu awe baba yetu wa Imani wa kila mwaminio na amjue Yesu Kristu. Tunaweza kurudi nyuma katika agano ya kale kuchunguza msitari maarafu. Mwanzo sura ya 22 tunaarifiwa kuhusu tukio ambapo Ibrahimu alikuwa tayari kumtoa sadaka mwanawe wa pekee Isaka kwenye mlima Moria, ambao ulikuwa ukalimisho wa mfululizo wa maajaribu ambaye hatimaye yangemfikisha kiwango cha kuitwa Baba wa Imani. Na sasa fungua aya 13 ya Waruni sura ya 4 na tusome kwa Pamoja. "Kwa maana ahadi ile ya kwamba atakuwa mrithi wa ulimwengu alipewa Ibrahimu na uzao wake, si kwa sharia bali kwa haki aliyohesabiwa kwa Imani. Ni dhahiri kuwa ahadi zote alizopewa Ibrahimu na Mungu kuhusu kurithi au kutwaa nchi ya ahadi kuanzia mlima Lebanoni hadi mto nchi Msri na kutoka bahari kuu hadi mto Efrati, ambayo Israel iliahidiwa kuwa itarithi, japo kufikia sasa ndoto hiyo haijatimilika. Mungu alimwahidi Ibrahimu nchi ya kurithi. Mungu alimwambia Ibrahimu kuwa uzao wake utakuwa kama mchanga wa ufuo wa bahari, kama vumbi la ardhini na kama nyota wa mbinguni. Katika ahadi hizo zote, msikilizaji wangu hatujapewa kipimo. Kile tunachoambiwa ni idadi kubwa ama sehemu kubwa ya... mchanga wa bahari, nyota za angani.

Kwenye aya 14 tunasoma kwamba, … **Maana Ikiwa wale wa sharia ndio warithi, Imani imekuwa bure na ahadi imebadilika, kwa sababu sharia ndiyo ifanyayo hasira, maana pasikuwepo sharia, hapana kosa. Kwa hiyo ilitoka katika Imani, iwe kwa njia ya neema ili kwamba ile ahadi iwe imara kwa wazao wote; si kwa wale wa torati tu, ila na kwa wale wa imani ya Ibrahimu, aliye baba yetu sisi sote. Kama ilivyoandikwa nimekuweka kuwa baba wa mataifa mengi**… huo ni msitari wa 16.

Kwa hiyo mtume Paulo anatuhitimishia somo hili kwa kumtumia Ibrahimu kama mfano. Yeye ndiye Baba wa Imani. Mpendwa naomba kutamatishia somo hili hapo

ili tuendelee kwenye Makala yajayo. Lakini kabla ya kuhitimisha nakuuliza je? Umempokea Kristu kuwa mwokozi wa roho yako? Ikiwa sivyo, wakati ni huu. Fanya uamuzi huo sasa ili usikose uzima wa milele na makao alioenda kutwandalia mwokozi Yesu Kristu.

Nitafurahi sana Ikiwa utachukua hatua ya kutubu dhambi zako na kumpokelea Kristo kuwa mwongozi wako. Ukifanya hivyo nakusihi utafute kanisa wanakohubiri Injili ya wokovu ya Yesu Kristo na ujiunge na waumini watakaokusaidia kuweka msingi madfhubuti wa wokovu wako.

Ninasubiri uchukue hatua hiyo, kisha uniandikie au nitumie ujumbe mfupi. Nitafurahi sana kuwasiliana nawe na hata kukupatia vijitabu na nakala ya agano jipya la Bibilia kukusaidia kuweka msingi imara wa Ukristo wako. Zaidi ya hayo, nitafurahia sana nitakapo pokea maaoni yako kukihusu kipindi hiki na hasa jinsi ya kukifaya kiwe cha manufaa zaidi kwako. Hiki kimekuwa kipindi cha Mwito nambari 1074. Naomba uwasiliane nami kupitia njia ya arafa ukipitia namba ifuatayo-: 0721 970 520 au 020 267 9842. Ikiwa unaishi Nairobi tunakukaribisha ututembelee kwenye studio zetu za TWR Kamburu Drive, off Ngong road, baada ya jumba la TOP PLAZA. Anwani yangu Ikiwa utaniandikia ni: kwa mtayarishi, Mwito, S.L.P.21514-00505, Nairobi. Waweza pia kuwasiliana nami kwa njia ya barua pepe ifwatayo, barua@twr.co.ke . Na basi kufikia hapo sina budi bali kulikunja jamvi langu kwa leo ninapokutakia baraka sufufu kutoka kwake Mungu wetu mtukuka. Juma lijalo tutaingia aya ya 1 ya sura ya 4 cha kitabu cha Warumi. Ni mwaandalizi wa kipindi hiki ndugu Charles Otunga ninayekuaga nikikutakia mbawazi zake Mungu wetu Mtukuka. Kwaheri.